



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII



CHUO CHA VIWANDA VYA MISITU

TANGAZO LA KUJIUNGA NA CHUO KWA MWAKA WA MASOMO 2023/2024

Chuo cha Viwanda vya Misitu (FITI) ni taasisi ya Serikali chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii (WMU). Chuo hiki kinapatika mtaa wa Viwanda, Kata ya Njoro Manispaa Moshi Kilomita 3 kutoka stendi kuu ya mabasi ya Moshi Mjini.

Chuo kinapenda kutoa taarifa kwa umma kuwa kimeanza kupokea maombi ya waombaji wapya ya kujinga na chuo kwa mwaka wa masomo 2023/2024. Muda wa kutuma maombi ni kuanzia tarehe **15 Mei, 2023** na mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **28 Julai, 2023**.

1. KOZI ZITOLEWAZO HAPA CHUONI

- (a) Astashahada ya awali ya Teknolojia ya Viwanda vya Misitu (NTA 4) mwaka mmoja
- (b) Astashahada ya Teknolojia ya Viwanda vya Misitu (NTA 5) mwaka mmoja
- (c) Stashahada ya Teknolojia ya Viwanda vya Misitu (NTA 6) mwaka mmoja

2. SIFA ZA MWOMBAJI

- (a) Astashahada ya awali ya Teknolojia ya Viwanda vya Misitu (NTA 4):** Mwombaji awe amehitimu kidato cha nne (O-Level) na ufaulu wa alama D katika masomo manne. Mawili kati ya masomo aliyofaulu yawe ni aidha Bilojia au Kemia au Fizikia au Hesabu au Jiografia. Masomo mengine mawili kati ya hayo aliyofaulu yawe siyo ya dini, ufaulu wa somo la kiingereza utakuwa kipaumbele katika uchaguzi;
- (b) Astashahada ya Teknolojia ya Viwanda vya Misitu (NTA 5):** Mwombaji awe na cheti cha kuhitimu astashahada ya awali ya Teknolojia ya Viwanda vya Misitu au astashahada ya awali ya ufugaji nyuki au astashahada ya awali ya misitu au fani nyingine inayolandana na hizo kutoka chuo chochote kinacho tambulika na NACTVET au awe na amehitimu kidato cha sit ana awe amesoma michepuo ya sayansi na kufaulu katika masomo mawili kwa alama ya E na S;
- (c) Stashahada ya Teknolojia ya Viwanda vya Misitu (NTA 6):** Mwombaji awe amehitimu astashahada ya Teknolojia ya Viwanda vya misitu au awe amehitimu na kufaulu fani nyingine yoyote ya sayansi inayolandana na hizo kutoka chuo kinacho tambulika na NACTVET;

3. JINSI YA KUTUMA MAOMBI

- (a) Mwombaji atatakiwa kujaza fomu kikamilifu na kuambatisha vielelezo vyote muhimu ikiwemo vivuli vya vyeti halisi, picha ya passport size 1 na taarifa za matokeo katika lugha ya Kiingereza. Endapo mwombaji atakuwa na ufadhili, uthibitisho wa maandishi kuhusu ufadhili huo utahitajika;
- (b) Ada ya fomu ya maombi ya kujiunga na chuo ni Tsh. 10,000.00 (elfu kumi tu) kwa Watanzania na Dola za Kimarekani 20.00 kwa wasio Watanzania;
- (c) Fomu za maombi zinapatikana kwenye tovuti ya Chuo (www.fiti.ac.tz) na maombi yote yatumwe kwa njia ya posta au kwa kufika moja kwa moja Chuoni au kwa barua pepe: admission@fiti.ac.tz
- (d) Mwombaji atatakiwa kulipia ada ya fomu ya maombi kwa *control number* tuu.
- (e) Ili kupata control number au kupata ufafanuzi wa jinsi ya kujiunga na chuo, mwombaji awasiliane na Afisa udahili wa chuo kwa namba za simu 0787676981.

4. TAHADHARI

- (a) Kwa mwombaji yeyote ambaye hatazingatia utaratibu uliotajwa hapo juu, maombi yake hayatafikiriwa;
- (b) Kwa mwombaji atakayewasilisha hati za kughushi atachukuliwa hatua za kisheria;
- (c) Mwisho wa kupokea maombi kwa awamu ya kwanza ni tarehe 23 Julai, 2023.

5. TAARIFA KWA WATAKAOCHAGULIWA

Majina ya wataochaguliwa pamoja na maelezo ya kujiunga na chuo yatawekwa kwenye tovuti ya Chuo <http://www.fiti.ac.tz>;

“WAOMBAJI WOTE WENYE SIFA MNAKARIBISHWA”

Imetolewa na:

Mkuu wa Chuo,
Chuo cha Viwanda vya Misitu,
S. L. P 1925, Moshi.
Tovuti: www.fiti.ac.tz